Kwa Nini Yesu Alikufa Msalabani?

na

Ellis P. Forsman

Kwa Nini Yesu Alikufa Msalabani?

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 17, 2011

Kwa Nini Yesu Alikufa Msalabani?

1 Wakor. 15:1-3

Picha kama za muigizaji Mel Gibson aliyeigiza "Uruma ya Kristo" iliyo zaliza mjadala mwingi.....

- Kwa kujali mtazamo wa picha yenyewe.
- Kwa kujali mchoro unaonyosha kushikwa na kusulubiwa kwake.

Wakati mwingine mjadala unabakia kwamba ni kwa sababu gani Yesu alikufa.

Je kifo chake kilikuwa cha bahati mbaya, madhara ya mafundisho yake ambayo hayaku kusudiwa?

Je yalikuwa mapenzi ya Mungu yaliyotambulika na kukubaliwa na Yesu kwa ziada?

Ujumbe wa injili uko wazi kwetu kwamba ni kwa nini Yesu alitufia, na kuna sababu ambayo mara nyingi haizingatiwi. Sasa hebu na tuangalie majibu ya Biblia kuhusu swali hili...

Kwa nini Yesu alikufa msalabani?

Alikufa ili ajitawadhe kwa ajili ya dhambi zetu.

Hii ndiyo kusudi kuu ya Injili. 1 Wakor. 15:1-3, *"Basi ndugu zangu nawaarifu ile injili niliyowahubiri, ambayo ndiyo mliyoipokea, na katika hiyo mnasimama, na kwa hiyo mna okolewa ikiwa mnayashika sana maneno niliyowahubiri, isipokuwa mliamini bure. Kwa maana naliwatolea hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko."*

Mateso yake kwa ajili ya dhambi zetu ili tabiriwa.

- Isay. 53:4-6, *"Hakika ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu; lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi kama kondoo tumepotea kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; na BWANA ameweka juu yake maovu yetu sisi sote."*

- Isay. 53:10-12, *"Lakini BWANA aliridhika kumchubua; amemhuzunisha; utakapofanya nafsi yake kuwa dhabihu kwa dhambi, ataona uzao wake, ataishi siku nyingi, ataona mazao ya tabu yake na kuridhika kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki atawafanya wengi kuwa wenye haki naye atayachukua maovu yao. Kwa hiyo nitamgawia sehemu pamoja na wakuu, naye atagawanya nyara pamoja nao walio hodari; kwa sababu alimwaga nafsi yake hata kufa, akahesabiwa pamoja na hao wakosao. Walakini alichukua dhambi za wutu wengi, na kuwa ombea wakosaji."*

Alikuwa mwanakondoo aliyechukua dhambi za ulimwengu. Yoh. 1:29, *"Siku ya pili yake amwona Yesu anakuja kwake, akasema tazama mwana kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu."*

Katika upendo, Mungu alimtoa kama mpatanishi wa dhambi zetu. 1 Yoh. 4:9-10, *"Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma mwana pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa yeye. Hii ndiyo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi akamtuma mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu."*

Kupitia mates ohayo alitupatanisha na Mungu. 1 Petr. 3:18, *"Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu, mwili wake akauawa, bali roho yake akahuishwa."*

Akitoa ukombozi kutoka dhambini kupitia damu yake ya thamani. 1 Petr. 1:18-19, *"Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu, mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mliyoupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo."*

Kifo chake hakikuwa cha bahati mbaya, bali ilikuwa ni sehemu ya mpango wa Mungu. Matend. 2:22-23, *"Enyi waume wa Israeli sikilizeni maneno haya: Yesu wa Nazareti mtu aliyedhihirishwa kwenu na Mungu kwa miujiza na ajabu na ishara ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake kati yenu, kama ninyi wenyewe mnavyojua; mtu huyu alipotelewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa, na kujua kwake tangu zamani, ninyi mkamsulubisha kwa mikono ya watu wabaya, mkamwua."*

Alikufa ili tuifie dhambi.

Sababu hii ya kifo chake mara nyingi haizingatiwi.

Ila, Petro anaweka wazi.

1 Petr. 2:24, *"Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi; tuwe hai kwa mambo ya haki, na kupigwa kwake mliponywa."*

- Alikufa kwa sababu ya dhambi zetu ili tuwe wafu kwa mambo ya dhambi.
- Alifia dhambi zetu ili tuweze hai kwa mambo ya haki.

Alikufa ili tuweze kufa! Na tunasoma kauli hizi kuwa:

- *"...kama tukifa pamoja naye..."* (2 Tim. 2:11)
- *"...kama tukifa pamoja na Kristo..."* (Wakol. 2:20)
- *"...kwa maana mlikufa...."* (Wakol. 3:3)
- *"...nasulubishwa pamoja na Kristo..."* (Wagal. 2:20).

Yesu alikufa sit u kuondoa dhambi, bali kutoa njia ambayo tuna weza kuifia dhambi pamoja naye, na kwa hiyo tuishi kwa haki.

Tusipoifia "ifia dhambi', kifo cha Yesu msalabani kili maliza kabisa kusudi lake? Alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, lakini je nasi tumezifia dhambi?

Kwa lugha nyingine...

Je Yesu amekufia bure?

Je umeifia dhambi?

Ni wakati gani ambapo Mungu anakuona kama...

- Unakufa pamoja na Kristo?
- Umesulubiwa pamoja na Kristo.
- Umeungana pamoja na Kristo katika kifo chake?
- Umeifia dhambi?

Paulo anaiweka wazi – tunapo batizwa!

Akiwaandikia Wakristo waliyoifia dhambi.

Waru. 6:1-2, *"Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije katika dhambi?"*

Paulo aliwakumbusha kuhusu ubatizo wao katika Kristo...

Walibatizwa katika mauti yake.

Waru. 6:3, *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake."*

Walizikwa pamoja naye kupitia ubatizo katika mauti yake.

Waru. 6:4, *"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."*

Utu wao wa kale ulisulubiwa pamoja naye.

Waru. 6:6, *"Mkijua neno hili, ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena."*

Kifo chao kimewaweka huru na dhambi, ikiwawezesha waishi na Kristo.

Waru. 6:7-8, *"Kwa kuwa yeye aliyekufa amehesabiwa haki mbali na dhambi. Lakini tukiwa tulikufa pamoja na Kristo, twaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye."*

Lazima wajitambue wenyewe kuwa wameifia dhambi.

Waru. 6: 11, *"Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu."*

Kama bado hatujabatizwa katika Kristo, hivyo bado hatujaifia dhambi!

Je unaishi kwa haki?

Hiyo ndiyo sababu umeifia dhambi.

1 Petr. 2:24, *"Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti; tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa."*

Ilikwamba muwe hai kwa Mungu.

Waru. 6:11, *"Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu."*

Ilikwamba msiruhusu dhambi imtawale ye yote.

Waru. 6:12, *"Basi, dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tama zake."*

Kwa mtoe viungo vyenu kwa silaha ya haki.

Waru. 6: 13, "*Wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi, bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha ya haki."*

Ili muwe watumwa wa haki.

Waru. 6: 16-18, *"Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajito nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake Yule mnaye mtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki. Lakini Mungu na ashukuriwe kwa maana mlikuwa watu wa dhambi lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu, ambayo mliwekwa chini yake; na mlipokwisha kuwekwa huru, mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki."*

Baada ya kuifia dhambi, tunauua mwili

Inahudumiwa na Roho wa Mungu.

- Waru. 8:13, *"Kwa maana kama tukiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwataka kufa; bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi."*
- Waef. 3:16, *"Awajalieni kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani."*

Tukitafuta kuutiisha mwili.

1 Wakor. 9:27, *"Bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa."*

Kuzikimbia tama za mwili.

1 Petr. 2:11, *"Wapenzi nawasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tama za mwili zipinganazo na roho."*

Kuua (kuweka mbali) matendo ya mwili ya dhambi.

Wakol. 3:5-9, *"Basi vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya, na kutamani, ndiyo ibada ya sanamu; kwa ajili ya mambo hayo huja ghadhabu ya Mungu. Katika hayo ninyi nanyi mlitembea zamani, mlipoishi katika hayo. Lakini sasa yawekeni mbali haya yote, hasira, na ghadhabu, na uovu, na matukano, na matusi vinywani mwenu. Msiambiane uongo, kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake."*

Baada ya kuifia dhambi, tunaishi kwa haki

Kuvaa utu mpya, uliofanya upya kwa mfano wa Kristo.

- Wakol. 3:10-14, *"Mkivaa utu mpya unaofanywa upya upate ufahamu sawa sawa na mfano wake yeye aliyeumbwa. Hapo hapana Myunani wala Myahudi, kutahiriwa wala kutokutahiwa, mgeni wala mshenzi, mtumwa wala mwungwana, bali Kristo ni yote katika yote. Basi kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu,watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, ,kichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi vivyo na ninyi. Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo, ndio kifungo cha ukamilifu."*
- Waef. 4: 22-32, *"Mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani unaoharibika kwa kuzifuata tama zenye kudanganya; na mfanywe upya katika Roho ya nia zenu; mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli. Basi uvueni uongo mkaseme kweli kila mtu na jirani yake; kwa maan tu viungo, kila mmoja kiungo cha wenzake. Mwe na hasira ila msitende dhambi jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka; wala msimpe ibilisi nafasi. Mwibaji asiibe tena, bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji. Neno lolote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanao sikia. Wala msimhuzunishe Yule Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi. Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu pamoja na kila namna ya ubaya; tena iweni wafadhi ninyi kwa ninyi, wenye huruma mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi."*

Kukuwa katika ujuzi wa kweli wa Kristo.

2 Petr. 1:5-9, "Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika imani yenu tieni wema, na katika wema wenu, maarifa, na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa, na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, upendo. Maana mambo haya yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo. Maana yeye asiyekuwa na hayo ni kipofu, hawezi kuona vitu vilivyo mbali, amesahau kule kutaswa dhambi zake za zamani."

Ni kwa kiasi gani tumetilia maanani juhudi hii? Kama ilivyo thibitishwa na:

Je! nimapenzi yetu kusoma na kujifunza katika ujuzi wa Kristo?

2 Petr. 3:18, *"Maana wakinena maneno makuu mno ya kiburi, kwa tama za mwili na kwa ufisadi huwahadaa watu walioanza kuwa kimbia wale wanaoenenda kwa udanganyifu."*

Ni juhudi zetu kuweka mbali dhambi na kumvaa Kristo katika maisha yetu?

Waru. 13:13-14, *"Kama ilivyo husika na mchana tuenende kwa adabu; si kwa ulafi na ulevi, si kwa ufisadi na uasherati, si kwa ugomvi na wivu. Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tama zake."*

Kama hatukazani kuweka mbali dhambi na tumvae Kristo, basi kifo chake kwa ajili yetu kilikuwa bure!

Hitimisho

Tunapozingatia kifo cha Yesu msalabani...

Tusifikirie tu kifo chake kama dhabihu kwa ajili ya dhambi zetu.

Lakini pia akitupatia njia tunayo weza kuifia dhambi na tukaishi kwa haki.

Neema ya Mungu katika Yesu haijatimia hadi tuishi kama tunavyo weza...

- Tito 2:11-12, *"Maana neema ya Mungu iwaokoyo wanadamu wote imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa ubaya na tama za kidunia, tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utaua, katika ulimwengu huu wa sasa."*
- Tito 2:13-14, *"Tukulitazamia tumaini lenye Baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu; ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu ili atukomboe na maasi yote na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema."*

Wale ambao ni Wakristo wameusulubisha mwili (Wagal 5:24; Waru. 6:6).

Je uko katika Kristo?